## Maswali

1. Ahabu alikuwa mfalme wa aina gani?
2. Mungu aliahidi nini?
3. Nini ilifanyika kwa vita?
4. Mungu alimchagua mfalme gani tofauti?
5. Nini ilifanyika kwa shamba la mizabibu la Nabothi?
6. Mbona Yehu hakuogopa Yezebeli?
7. Nini ilifanyika kwa Yezebeli?
8. Watu waovu waliadhibiwa namna gani?
9. Yehu aliwadanganya waabudio Baali namna gani?
10. Mbona Israeli walikuwa dhaifu?

## Majibu

1. Ahabu alikuwa mfalme muovu asiyesikiliza Mungu na aliabudu sanamu.
2. Mungu aliahidi kwamba baada ya Ahabu kufa, familia yake yote itauwawa kwa sababu ya uovu wao.
3. Ahabu aliuwawa vitani kwa kupigwa upindi wa mshale.
4. Mungu alimchagua Yehu amri mkuu wa jeshi kama mfalme.
5. Yehu alipata Yoramu na Ahazia kwa shamba la mizabibu la Nabothi na akawauwa wote kwa sababu walikuwa waovu.
6. Yehu hakumuogopa Yezebeli kwa sababu alijua ako anafanya kazi aliyotaka Mungu. Mungu alikuwa naye.
7. Yezebeli alitupwa kupitia kwa dirisha, akakanyagwa na farasi wa Yehu na mbwa zikamkula.
8. Vichwa vya watu waovu vilikatwa.
9. Yehu alijifanya anataka kuabudu Baali nao, walipofika aliwauwa wote.
10. Israeli ilikuwa dhaifu kwa sababu mfalme wao Yehu hakufuata sheria za Mungu. Hakuwafundisha vizuri.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1    Mwaka wa 2

# 25 Mfalme Yehu

## Marejeo

1 Wafalme 19:16, 21-24;  2 Wafalme 9 na 10

## Kiini cha somo

Kuona kwamba Mungu hutimiza ahadi zake.

## Maneno maalum

1. Mfalme Ahabu + Israeli + abudu Baali + sanamu + ovu + familia yote + wote watakufa.
2. Vita + hakusikiza + uwawa kwa gari + mbwa za lamba damu + ahidi + Yoramu + ovu.
3. Elisha + mfalme mwingine + Yehu + timiza ahadi + Yuda naye muovu.
4. Yoramu + Ahazia + Yehu + alikuwa kwa shamba la mizabibu la Nabothi + amani + Yezebeli aabudu Baali + Yehu aliwapiga.
5. Yezebeli + uso na nywele + orofa + ogopa + nani ako upande wangu + tupa chini + kufa + farasi zilikanyaga + mbwa zilikula.
6. Wana wa Ahabu + Samaria + uwawa + Yehu apeleka vichwa + Mungu ametenda alichoahidi + waovu waaadhibiwa.
7. Wana wa Ahazia + uwawa + waabudu Baali + wauwawa wote + hekalu za bomolewa.
8. Yehu afanya kazi yake vizuri + familia ya Ahabu + waabudio Baali + hakufuata sheria vizuri + Israeli dhaifu + nchi inachukuliwa.

**25.1** Ahabu mfalme wa Israeli hakutaka kumsikiliza Mungu. Aliabudu Baali aliyekuwa sanamu. Aliyetengenezwa kutoka kwa miti au jiwe au chuma. Ahabu alikuwa muovu sana. Familia yake yote ilimuacha Mungu. Mungu aliahidi kwamba Ahabu, Yezebeli mkewe na familia yake yote watakufa kwa ajili ya uovu wao. (soma 1Wafalme 21:21-24).


**25.2** Ahabu alikuwa tayari kwa vita. Nabii wa Mungu alimwonya kwamba atakufa lakini hakusikia. Huyu mfalme muovu aliuwawa wakati alikuwa kwa gari. Jeshi lake lilishindwa. Walipoosha damu kutoka kwa gari lake, mbwa walilamba hiyo damu sawa sawa na vile Mungu alikuwa ameahidi. Mwanawe Yoramu alianza kutawala na akawa muovu kama baba yake na mama yake.

**25.3** Nabii aliambia nabii kijana aende atawaze mfalme mwingine. Mungu alikuwa amemchagua Yehu amri mkuu wa jeshi. Jeshi lote lilimuunga Yehu waliposikia nabii akisema kwamba atakuwa mfalme. Mungu alitaka Yehu atimize ahadi alizokuwa ameahidi Ahabu na familia yake. Uovu wa Ahabu ulikuwa umeenea mpaka nchi ya Yuda pia. Binti wake alikuwa ameolewa kwa mfalme Ahazia wa Yuda. Alikuwa muovu kama mama yake Yezebeli. Aliwafundisha watu kuabudu Baali badala ya Mungu. Mungu hakukubali hii familia ya watu wasio na utawa kutawala.

**25.4** Yehu alienda kumuona Yoramu na Ahazia mfalme wa Yuda pia alikuwa huko. Walikutana kwa shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli aliyekuwa ameuwawa na Ahabu na Yezebeli. Yoramu aliuliza kama Yehu alikuwa amekuja kwa amani. Yehu alimjibu, “Hakutakuwa na amani kama mama yako Yezebeli anafundisha watu kuabudu Baali!” Yoramu alijaribu kutoroka lakini Yehu akampiga kwa upindi wa mshale. Mwili wake ulikaa kwa shamba la Nabothi. Ahazia pia aliuwawa na Yehu.

**25.5** Yehu alienda kumuona Yezebeli. Yezebeli alijipaka rangi kwa uso wake na kutengeneza nywele ili aonekane mrembo na wa nguvu. Alimchungulia Yehu kwa dirisha la orofa na kampazia sauti, “Kuna amani kwa kumuuwa bwana wako?” Yehu hakumuogopa, anaye akasema kwa sauti, “Nani ako upande wangu?” Watumishi wa Yezebeli wawili au watatu waliangalia nje kwa dirisha. Yehu akawambia wamtupe Yezebeli nje kupitia dirishani, walimtupa na akafa. Farasi wa Yehu wakamkanyaga, mbwa wakamla. Kila kitu kikakuwa vile Mungu alivyomwambia Ahabu.





**25.6** Ahabu alikuwa Samaria na wana sabini. Watumishi wao waliogopa Yehu kwa hivyo wakauwa hao wana wote na kupelekea Yehu vichwa vyao. Yehu aliita watu wote pamoja. Akachukuwa vichwa vya wana wa Ahabu na akawambia, “BWANA Mungu amefanya alichosema atafanya, watu hawa waovu wameadhibiwa.”

**25.7** Tena Yehu aliuwa wana 42 wa mfalme Ahazia wa Yuda. Yehu aliwadanganya watu kwamba wakuje wote pamoja ili waabudu Baali sio Mungu. Aliwauliza wakutane naye, aliwauwa wote na akaaribu hekalu la kuabudia Baali.

**25.8** Yehu alifanya vizuri kazi aliyopewa na Mungu. Aliuwa familia ya Ahabu na watu wote walioabudu Baali.Mungu alifurahia hiki kitendo. Ingawaje Yehu naya hakufuata amri za Mungu vizuri. Hakuwaongoza watu kufuata njia za Mungu. Kwa hiyo Israeli wakawa wadhaifu na nchi zingine zikachukuwa sehemu ya nchi yao.